TANGAZA NASI:
0683 378 522
0765 142 207
uhuruadvert@gmail.com



# TMA: Wananchi chukueni tahadhari ya mvua

**Na REHEMA MOHAMED**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imewataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mtaalamu wa Hali ya Hewa wa TMA, Alfred Kondowe, alipozungumza na gazeti hili kuhusu mvua inayoendelea kunyesha mikoa mbalimbali na hatua ambazo wananchi wanapaswa kuzichukua.

Kondowe alisema hivi karibuni mamlaka hiyo ilitoa taarifa iliyoonesha mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Njombe, Songea, Mbeya na Ruvuma, itanyesha mvua kubwa Februari 16 na 17, mwaka huu.

"Maeneo hayo ni yale yanayopata msimu mrefu wa mvua, kwa msimu mmoja na kutoa tahadhari kwa wananchi kujikinga na mvua hiyo kubwa na majanga yanayoweza kutokea," alisema.

Mtaalamu huyo aliyataja maeneo mengine yaliyotabiriwa kunyesha mvua kubwa Februari 17, mwaka huu, ni ukanda wa Ziwa Victoria, katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Simiyu, Mara na Shinyanga.

"Tahadhari za kuchukua dhidi ya mvua hutegemea na utofauti wa maeneo husika. Mfano maeneo yenye mvua kubwa watoto wanaokwenda shule tunatoa tahadhari kwa wazazi wawasindikize kuhakikisha wanafika salama na uwepo wa mawasiliano kati ya wazazi na walimu," alisema Kondowe.

Aliongeza kuwa: "Wale wanaokwenda kazini wabebe mwavuli kuepuka kusimama muda mrefu kusubiri mvua kuisha. Kwa ujumla katika nchi yetu mwezi huu wa pili kuanzia tarehe 16, kunakuwa na kuimarika kwa mifumo ya hali ya hewa na maeneo mengi yataendelea kupata mvua tunayoiona."

Kwa mujibu wa Kondowe, mvua hiyo itaendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini kuelekea mwishoni mwa Februari, mwaka huu, kwa maeneo ambayo hupata mvua za masika.

Aliyataja baadhi ya maeneo hayo ni ya Pwani ya Kaskazini, mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga, visiwa vya Unguja na Pemba, Zanzibar na Morogoro Kaskazini, Arusha, Kilimanjaro na Manyara na ukanda wote wa Ziwa Victoria.

Mtaalamu huyo alibainisha Mikoa ya Kigoma Kaskazini, mvua za masika zitaanza wiki ya nne ya Februari kwa upande wa Ziwa Victoria na kusambaa maeneo mengine kwenda wiki ya kwanza na ya pili ya Machi.

"Kuna uwezekano mkubwa wa mvua inazonyesha hivi sasa kuungana na ya masika. Ninatoa wito kwa wananchi kuendelea kufuatilia taarifa tunazozita TMA, kupata ushauri wa kisekta katika maeneo yao, waendelee kuwa salama wao na mali zao," alisema.

Pia, aliwasihi wakazi wa mabondeni kuchukua tahadhari, kufuatilia taarifa za hali ya hewa na kusikiliza mamlaka husika katika maeneo yao.

"Tunapotoa taarifa mkoa fulani unatarajiwa kutokea mvua kubwa, wananchi wa eneo husika wachukuwe tahadhari, wajiandae," alisisitiza.

# Balozi Kusiluka atoa maagizo kwa wataalamu wa TEHAMA

**Na MWANDISHI WETU**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, amesema wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanatumia taaluma zao, ujuzi na ubunifu kwa maslahi mapana ya taifa.

Aidha, amewataka wataalamu hao kuhakikisha wanatumia teknolojia hiyo au kusimamia matumizi ya teknolojia, kuhakikisha inailetea nchi maendeleo, badala ya uhalifu.

Balozi Kusiluka alisema hayo, jijini Arusha, juzi alipofungua kikao kazi cha Sita cha Serikali Mtandao 2026, kinachofanyika kwa siku tatu kilichobebwa na kaulimbiu isemayo; 'Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao.

"Mategemeo yangu katika kikao kazi hiki pia mtajadili kwa kina namna bora ya kutumia teknolojia hizi, kulinda maslahi, mila na desturi ya taifa letu," alisema.

Balozi Kusiluka alisisitiza kuwa, wataalamu wa TEHAMA wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanatumia taaluma zao, ujuzi na ubunifu kwa maslahi mapana ya taifa.

"Nitoe wito kwenu nyote kuhakikisha tunatumia teknolojia hii au kusimamia matumizi ya teknolojia hii, kuhakikisha inatuletea maendeleo, badala ya uhalifu," alisema.

Pia, alisema TEHAMA ni kipaumbele cha serikali na hata Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wanaitumia kwa kiwango kikubwa katika utekelezaji wa majukumu.

Balozi Kusiluka aliipongeza e-GA kwa kubuni na kusanifu mifumo mbalimbali ya TEHAMA ambayo inarahisisha utendaji kazi wa kila siku serikalini.

"Tuliokuwa katika utumishi wa umma tangu zamani tunaona, kulikuwa na vikwazo vingi wakati tunataka kuanza kusanifu mifumo yetu, kuna watu wakasema hatutaweza, lakini sasa tumeweza, niwapongeze e-GA, niwasisitize kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolijia tusiachwe nyuma," alisisitiza Katibu Mkuu Kiongozi huyo.

Aidha, alisema serikali inathamini mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya TEHAMA na kuhimiza kuendelezwa kwa ushirikiano wawahudumie wananchi kikamilifu.

Akizungumzia kaulimbiu hiyo, Balozi Kusiluka alibainisha kuwa, inaakisi kikamilifu mwelekeo wa serikali wa kuhakikisha huduma za umma zinakuwa bora, zinapatikana kwa wakati, kwa uwazi, kwa usalama, kwa urahisi na haraka na bure ama kwa gharama nafuu kwa njia ya teknolojia.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba alisema mamlaka hiyo imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao.

Alifafanua kuwa, inafanya hivyo, kwa kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanakuwa shirikishi, salama, yanazingatia sheria, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao, kuleta tija katika utoaji huduma kwa wananchi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019.

Mhandisi Ndomba alimshukuru Rais Dk. Samia kwa jitihada zake za kuwekeza katika sekta ya TEHAMA na kuiwezesha mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yake, yakiwemo ujenzi wa mfumo unaowezesha mifumo ya serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa, ujulikanao kama Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB).

Aliongeza eGA imeimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA serikalini, kuendeleza mtandao wa mawasiliano ya serikali na kusimamia vituo vya kitaifa vya kuhifadhi datavinavyowezesha taasisi za umma kuendesha mifumo yao kwa usalama.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio bado kuna changamoto zinazopunguza ufanisi utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, zikiwemo uhaba wa wataalamu wabobezi wa TEHAMA katika maeneo mbalimbali na kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani na kuhitaji maofisa TEHAMA kujengewa uwezo mara kwa mara kukabili mabadiliko hayo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), Dk. Said Seif Said alisema ushirikiano baina ya serikali, taasisi za mawasiliano na wadau wa teknolojia unaendelea kuimarisha mageuzi ya kidijitali.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Toba Nguvila, amesema mkoa huo utaendelea kuwa kinara wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

## Dereva bajaji adai kukamatwa wakizungumzia kauli ya CHADEMA

**Na MWANDISHII WETU**

DEREVA bajaji P7, ambaye ni shahidi wa siri wa jamhuri, amedai alikamatwa na polisi, katika kijiwe cha bajaji, Mromboo, jijini Arusha na wenzake wakizungumzia kauli ya CHADEMA ya kupanga kuzuia uchaguzi mkuu, mwaka jana.

Shahidi huyo wa 11, alidai hayo Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Ndogo ya Dar es Salaam, jana, mbele ya Jopo la Majaji watatu Dunstan Ndunguru, James Karayemaha na Ferdinand Kiwonde, alipotoa ushahidi katika kesi ya uhaini inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Thawabu Issa, kutoa ushahidi, shahidi huyo mwenye umri wa miaka 26, alidai Aprili 3, mwaka jana, akiwa kazini kijiwe kwa Mromboo, katika mazumgumzo ya kawaida na wenzake, mmoja wao alikuja na hoja ya CHADEMA.

"Katika eneo hilo kuna huduma mbalimbali za kijamii, zikiwemo mama lishe na maduka ya mahitaji ya nyumbani, kuna mtu aliibua mazumgumzo kuhusu CHADEMA kujipanga kuzuia uchaguzi mkuu mwaka jana.

Shahidi huyo alidai wakiwa wanaendelea kubishana, alipata hamasa kupitia hayo maneno yaliyotolewa na chama hicho, hivyo aliingia katika mtandao wa YouTube kwa kutumia simu janja kusikiliza.

Alidai baada ya muda mfupi, walifika askari ambao waliwaeleza wapo chini ya ulinzi, hivyo kuna baadhi ya walikimbia na kubaki yeye na mwezake.

"Tulipelekwa Kituo cha Polisi Murieti, Arusha ambako tulikaa dakika 45, kisha tukapelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Mjini Kati, Arusha, Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa (RCO). Niliambiwa kuwa ninakabiliwa na kosa la kutaka kufanya fujo, niliandika maelezo na kupelekwa mahabusu," alidai.

Shahidi alidai siku iliyofuata, alifuatwa na ndugu zake ambao walimdhamini na kutakiwa kuripoti polisi, jambo ambalo alilitekeleza kadri alivyopangiwa tarehe.

"Aprili 17, mwaka jana, baada ya kufika kituoni kama kawaida niliambiwa niandike maelezo upya," alidai.

***Kesi itaendelea na kusikilizwa leo.***

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
YAH:SHAURI LA MIRATHI NA 17/2026
MWOMBAJI..................
ELYNESS GEORGE BAKEBULA
DHIDI YA
MAREHEMU..........CELESTINE EMANUEL MAHUBI
Watu wote wanaodai kua na Uhusiano wowote, maslahi yoyote ya marehemu CELESTINE EMANUEL MAHUBI wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya ivyo mnamo tarehe 03.03.2026 kabla mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Zingatia endapo kuna yoyote mwenye pingamizi awasilishe kabla ya tarehe tajwa.
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
BUSWELU
MWANZA
9869

SHERIA YA KUMILIKI ARDHI
(SURA 117)
KUPOTEA KWA LESENI YA MAKAZI
NAMBA YA LESENI: ILA014588
MMILIKI:ULRICK JOHN MSAMI
NAMBA YA KIWANJA:ILA/UKG/MRK33/76
MWOMBAJI:ULRICK JOHN MSAMI
TAARIFA IMETOLEWA
kwamba leseni ya Makazi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa leseni ya makazi mpya badala yake,iwapo hakuna pingamizi kw muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.
Leseni ya Makazi ya asili ikionekana irudishwe kwa msajili wa Nyaraka Msaidizi S.L.P 20950 Ilala, Dar es salaam
G.R Mlotwa
Afisa Mteule wa Leseni za Makazi
Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam
9871

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 3716 OF 2025**
In the Matter of the Estate of the Late **PETRO JAMES MAULANA**
And
In the Matter of Application for letters of administration by **GRACE FRANCIS WESTERBERG**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**
All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named
Deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit
Before the grant of probate (or letters of administration) is made to the
Above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 09 day of February **2026**
Dated at **DAR ES SALAAM** this 17 day of 2, **2026**
SENIOR Resident Magistrate
9872

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA – MWANZA
Shauri la Madai Na. 373 ya 2025
Mdai: .................RAMADHANI YUSUPH SIMBANGENI
Dhidi ya
Mdaiwa:........................ DICKSON WANGWE
KWA: DICKSON WANGWE
POPOTE PALE ULIPO
KUITWA SHAURINI
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)
Kwa kuwa ameleta mdai dhidi yako kwa hiyo shauri hili limepangwa kwaajili ya kusikilizwa siku ya IJUMAA mnamo tarehe 20/02/2026 majira ya 2:30 Asubuhi mbele ya Mhe.N.W. TUNGARAZA – Hakimu Mkazi katika kituo cha Mahakama ya Mwanzo Ilemela Mkoa wa Mwanza. Kwa kuwa siku hiyo ni siku ya HUKUMU ya shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako n vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Alhamisi ya February 12,2026
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA
9873

SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI 1999
KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI
NA TAARIFA YA KUMILIKI KIWANJA
SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI YA MWAKA 1999 (SURA 113)
KUSUDIO LA KUMILIKISHA BARUA YA TOLEO YA HAKI MILIKI ARDHI
MMILIKI ALIYEANDIKISHWA :ATHUMANI KISSANI
DAR ES SALAAM
ARDHI:KIWANJA NA 38 KITALU 'L'MBAGALA
MWOMBAJI:ABDUL ATHUMANI KISANI na KARIM ATHUMANI SINANI (msimamizi wa mirathi ya ATHUMANI HALFANI KISANI (marehemu)
DAR ES SALAAM
Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Temeke inakusudia kuwaandalia Nyaraka ya umiliki Ndugu ABDUL ATHUMANI KISANI NA KARIM ATHUMANI SINANI ambao ni wasimamizi wa mirathi ya ndugu ATHUMANI KISSANI lakini kwenye mfumo wa kodi anasomeka ndugu BORA ATHUMANI kwahiyo kabla hatujaendelea na utaratibu, Ofisi inamtaka ndugu BORA ATHUMANI au yeyote anayemfahamu afike ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Temeke Ndani ya siku 28 endapo atashindwa kufika ndani ya muda huo ofisi itaendelea na utaratibu unaofuata.
Salimu Shedaffa
**AFISA ARDHI MTEULE**
**HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE**
9874